TAASISI YA UTAFITI WA MASUALA YA UCHUMI NA MAMBO YA JAMII (ESRF)

WARSHA YA MALENGO YA MILENIA BAADA YA MWAKA 2015

Dkt. KHATIBU G.M.KAZUNGU

IMETOLEWA KATIKA CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI (VETA) MTWARA

4 DESEMBA 2012

Muhtasari

1. Utangulizi: Malengo ya Millenia
2. Mafanikio yaliyofikiwa hadi mwaka 2008
3. Changamoto
4. Baada ya 2015
5. Lengo la Mashauriano ya Kitaifa
6. Jukumu la ESRF katika Mchakato wa Baada ya 2015
7. Malengo na Mategemeo ya Warsha
8. Mwongozo
9. Hitimisho

1:Utangulizi: malengo ya milenia

- malengo ya milenia ni malengo ya maendeleo yanatoa mwongozo unaowezesha ufuatiliaji wa vigezo vya maendeleo katika nchi zote duniani kuanzia mwaka 1990 hadi 2015
- Malengo haya ambayo yalibuniwa mwezi Septemba mwaka 2000, yanaijumuisha Tanzania kama mojawapo ya mataifa 189, ambayo yaliafiki malengo haya katika Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa iliofanyika 2000
- Malengo ya Milenia ni manane (8), na yanazitaka nchi zilizoendelea na zinazoendelea kufanya kazi kwa ushirikiano ili kujenga dunia ambayo inapambana na umaskini, njaa na maradhi, yenye matumaini makubwa ya kuishi kwa kina mama na watoto wachanga, yenye kuhakikisha upatikanaji wa elimu ya msingi kwa watoto, fursa sawa kwa wanawake na mazingira bora

1:Utangulizi: malengo ya milenia

- Kitaifa, malengo haya yameainishwa katika mikakati ya maendeleo ya kitaifa kama:-
  - MKUKUTA I na II,
  - MKUZA kwa Zanzibar.
  - Mkakati wa mashirikiano kati ya Tanzania na nchi wafadhili (JAST, 2006)
  - Mpango wa maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2011/12-2015-16

2:Mafanikio yaliyofikiwa hadi mwaka 2008

- Tanzania ni kati ya nchi zilizoitikia wito wa Malengo ya Milenia, na imefanya vizuri katika maeneo mengi, ingawaje matokeo katika baadhi ya maeneo sio ya kuridhisha. Kwa mfano:
- Umasikini wa Huduma Muhimu (Basic Needs Poverty) umepungua toka asilimia 39 katika mwaka 1990 kwenda asilimia 36 katika mwaka 2000 na katika mwaka 2008 ulikuwa ni asilimia 34. Lengo kwa Tanzania ni kufikia asilimia 19.5 ifikapo mwaka 2015.
- Uandikishwaji wa watoto katika shule za msingi umeongezeka toka asilimia 54 katika mwaka 1990 kwenda asilimia 59 katika mwaka 2000 na kuwa asilimia 97 katika mwaka 2008. Lengo ni kufikia asilimia 100 katika mwaka 2015.
- Vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka watoto 115 katika 1000 (mwaka 1990) kwenda 99 katika watoto 1000 (mwaka 2000) na kuwa 68 katika 1000 mwaka 2008. Lengo ni kufikia vifo 38 katika watoto 1000 ifikapo mwaka 2015.

2:Mafanikio yaliyofikiwa hadi mwaka 2008

- ***Lengo Kuu: 1: Kupunguza na kuondoa ufukara na njaa (Eradicate extreme Poverty and Hunger)***
- **Malengo mahsusi:**
  - Kupunguza idadi ya watu wanaoishi kwa kipato chini ya USD 1 kwa siku kwa nusu kati ya 1990 na 2015
  - Kufanikisha upatinaji wa ajira yenye tija na hadhi kwa wote, pamoja na wanawake na vijana.
  - Kupunguza nusu ya asilimia ya watu wanaoathirika na njaa kati ya 1990 and 2015.

3:Mafanikio yaliyofikiwa hadi mwaka 2008: Lengo 1

- **Mafanikio**
- Kupungua kwa watu waishio katika kiwango cha chini ya dola moja kwa siku kutoka 35.7% mwaka 2001 hadi 33.6% mwaka 2007
- umaskini wa chakula ulishuka toka 18.7% mwaka 2001 hadi 16.6% mwaka 2007
- Zaidi ya ajira mpya 437,205 zilipatikana mwaka 2008 (sawa na 43.7% ya matarajio ya nafasi milioni 1 ifikapo 2010) katika sekta rasmi, sekta binafsi na kujiajiri

2:Mafanikio yaliyofikiwa hadi mwaka 2008: Lengo 2

- ***Lengo Kuu 2: Kufanikisha elimu ya msingi kwa wote (Achieve Universal Primary Education)***
- Malengo mahsusi: Kuhakikisha kuwa ifikapo 2015, watoto mahali pote, wakike na wakiume wanaweza kumaliza elimu yote ya msingi
- **Mafanikio**:Uandikishaji wa watoto umekua kwa wastani toka 80.7% mwaka 2002 hadi 97.7% mwaka 2007

2:Mafanikio yaliyofikiwa hadi mwaka 2008: Lengo 3

- ***Lengo 3: Kuinua haki za kijinsia na kuwezesha wanawake (Promote Gender Equality and Empower Women)***
- **Malengo mahsusi:**
- Kuondoa tofauti ya kijinsia katika elimu ya msingi na upili angalua ifikapo 2005, na katika ngazi zote za elimu si baada ya 2015
- **Mafanikio**: Elimu ya Msingi= uwiano ni 50/50
- Elimu ya juu = KE ni 34% kutoka 20% miaka ya 1990. (TCU, 2010)

2:Mafanikio yaliyofikiwa hadi mwaka 2008: Lengo 4

- ***Lengo Kuu 4: Kupunguza vifo vya watoto (Reduce child mortality)***
- **Malengo mahsusi**
- Punguza kwa kiwango cha mbili ya theluthi (2/3) vifo vya watoto waliochini ya miaka mitano kati ya 1990 na 2015.
- **Mafanikio:** Vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka 5 vimepungua kwa 24%
- Vifo vya watoto wachanga vimepungua kwa 31% toka vifo 99 hadi 68 kwa kila watoto wachanga 1000

2:Mafanikio yaliyofikiwa hadi mwaka 2008: Lengo 5

- ***Lengo Kuu 5: Kuboresha afya ya uzazi (Improve maternal health)***
- **Malengo mahsusi:**
- Kupunguza kwa robo tatu wastani wa vifo katika uzazi kati ya 1990 na 2015.
- Fanikisha ufikishwaji wa afya wa uzazi kwa wote ifikapo 2015
- **Changamoto:** Vifo vya kina mama wakati wa uzazi, Kiwango bado ni juu. Vifo ni 578 katika kila wazazi 100,000 kwa mwaka
- Uzazi unaohudumiwa na wahudumu wa afya (wakunga wataalam) TZ Bara - 63% ya wanawake walipata huduma ya kitalaam hadi mwaka 2007
- Kwa mwaka 2007, Uzazi wa mpango ulifikia 20%

2:Mafanikio yaliyofikiwa hadi mwaka 2008: Lengo 6

- ***Lengo Kuu 6: Kupambana na VVU na UKIMWI, Malaria na maradhi mengine***
- **Malengo mahsusi**
- Kusimamisha maambukizi ya VVU na kuenea kwa UKIMWI ifikapo 2015
- Kufanikisha kwa tiba za VVU na UKIMWI kwa wote ifikapo 2010
- Kupunguza kuenea kwa malaria na maradhi mengine na kusimamisha kabisa ifikapo 2015.
-

2:Mafanikio yaliyofikiwa hadi mwaka 2008: Lengo 6

- **Mafanikio**
- Viwango vya maambukizi ya HIV vimeshuka kwa wanawake na wanaume toka wastani wa 7.7% mwaka 2004 hadi 6.3% kwa 2007, ingawa wanawake wa makundi rika bado wana viwango vya juu
- Vituo vya VCT vimeongezeka kutoka520 (mwaka 2004) hadi 1646 (mwaka 2007) = ongezeko la asilimia 217%
- Viwango vya malaria vimeshuka toka wagonjwa 31,603 malaria kwa kila watu 100,000 mwaka 2003 hadi 27,030 mwaka 2006.
- 24.8 % ya watoto Tz wamelala kwenye chandarua chenye dawa yakinga (ITN).

2:Mafanikio yaliyofikiwa hadi mwaka 2008: Lengo 6

- **Mafanikio**
- Idadi ya wagonjwa wa TB kwa kila watu 100,000 imeshuka toka 186 mwaka 2004, hadi 164 mwaka 2006 na 158 mwaka 2007
- Tiba ya waliopata TB imeongezeka toka 81.33% mwaka 2004 hadi 84.8% mwaka 2008 karibu na kiwango cha dhahabu cha WHO cha 85%

2:Mafanikio yaliyofikiwa hadi mwaka 2008: Lengo 7

- ***Lengo Kuu 7: Kuhakikisha mazingira usalama endelevu wa mazingira***
- **Malengo mahsusi:**
  - Ainisha misingi ya maendeleo endelevu katika sera na programu za kitaifa ili kubadilisha kuendelea kwa kuharibika kwa mazingira
  - Punguza upotevu wa bayoanuai kwa kiwango kikubwa ifikapo 2010
  - Punguza kwa nusu, asilmia ya watu wasiopata maji safi na salama na ifikapo 2015.
  - Ifikapo 2020 kuboresha maisha ya angalau wakazi wa mijini milioni 100

2:Mafanikio yaliyofikiwa hadi mwaka 2008: Lengo 7

- **Changamoto**
  - uwezo ya kufikia 74 % ya wakazi vijijini kwa maji safi na salama ifikapo 2015 ni ndogo.
  - Asilimia 70% ya wakazi wa mijini bado wanaishi katika maeneo yasiyopimwa na hafifu

2:Mafanikio yaliyofikiwa hadi mwaka 2008: Lengo 8

- ***Lengo Kuu 8: Kuendeleza mashirikiano ya kimataifa kwa ajili ya maendeleo***
- **Mafanikio**
- Ni vigumu kuainisha taarifa za kiujumla katika lengo hili lakini mazingira wezeshi kufanikisha malengo mahsusi haya yanajitikeza katika Nyanja mbalimbali, kwa mfano:
  - Budget support

3: Changamoto

- Viwango vya umaskini viko juu zaidi kwa jamii za vijijini kuliko walio mijini
- Tofauti kimikoa – kwa mfano kwa watoto waliodumaa kwa Dar es Salaam ni 17% percent wakati kwa Lindi ni 54%
- Mazingira ya ufundishaji hasa shule za vijijini
- Huduma kwa wanafunzi – hasa kwa Sekondari
- Uduni wa miundo mbinu hasa maeneo ya vijinini

4:Baada ya 2015

- Mnamo Septemba 2010 Mkutano wa ngazi ya juu wa kimataifa uliitishwa ili kupitia maendeleo ya malengo ya millennia na kukubaliana kuhusu mpango kazi wa kuhimiza kukamilisha utekelezaji ifikapo 2015. Mkutano huu uliagiza mfumo wa Umoja wa mataifa kuendelea kutaarifu mijadala ya kimataifa kuhusu maendeleo na kuongoza majadiliano katika ngazi hii kuhusu ajenda ya baada– ya -2015.
- Kwa kuwa sasa hivi tunakaribia kufikia mwaka wa Malengo ya Milenia – mwaka 2015 (maana bado takribani miaka 3), na kwa kuwa baadhi ya nchi bado hazielekei kuyafikia Malengo ya Milenia ifikapo 2015 kama tunavyotegemea, watu na taasisi mbalimbali duniani wameshaanza kujadili na kujiuliza – kitatokea nini baada ya mwaka 2015!
- Wengine wameulizia nini kifanyike baada ya mwaka 2015 ili kuongeza kasi na kutoa msukumo wa maendeleo duniani! nk.

4:Baada ya 2015

- Maswali hayo yamepelekea serikali yetu kuagiza kuwa wadau mbalimbali katika nchi yetu washirikishwe katika majadiliano hayo ili tuweze kutoa vipau mbele kitaifa na kupanga mikakati endelevu ambayo wadau wenyewe wanaamini kuwa itakuwa na ufanisi. Taarifa itakayotokana na majadiliano haya, itakuwa mchango wa Tanzania katika kuandaa mikakati mipya na malengo mapya tunayoamini yatatoa msukumo wa kimaendeleo duniani kote, hususani katika nchi husika.

5:Lengo ya mashauriano ya kitaifa

- Lengo la mashauriano ya kitaifa ni kuchochea mjadala ya wadau mbalimbali kuhusu ajenda ya maendeleo ya baada- ya- 2015 kwa kutoa msingi wa uchambuzi, mchango na mawazo yatakayosaidia katika yafuatayo:
  - Kujenga taswira ya kimataifa kuhusu 'hali ya baadaye tunayoitaka' kwa mapendekezo madhubuti kwa serikali, mashirika ya kijamii na wadau wote wa maendeleo;
  - Kusikia sauti za maskini na makundi yaliyowekwa pembezoni na kuwezesha michakato ya utetezi wa masuala yao ;
  - kutambua na kuchambua masuala muhimu yanayoathiri maendeleo baada ya 2015
  - kushawishi michakato ndani ya serikali ioane na mategemeo ya mashirika ya kijamii katika ajenda ya maendeleo ya baada ya 2015.

6:Jukumu la ESRF katika Mchakato wa Baada ya 2015

- Katika kutekeleza Mchakato huo, Taasisi ya Utafiti wa Mambo ya Uchumi na Jamii (Economic and Social Research Foundation – ESRF) imeombwa kusimamia majadiliano hayo katika maeneo yafuatayo: Serikli za Mitaa (LGAs), Asasi za Kiraia (CSOs), Watoto, Wazee, na Wanawake wadogo (young women).
- Yako maeneo mengine ambayo wameombwa taasisi zingine kusimamia majadiliano ya wadau wa maeneo hayo. Majadiliano yanayosimamiwa na Taasisi ya Utafiti wa Mambo ya Uchumi na Jamii (ESRF) yanaendeshwa katika kanda 7 za Tanzania kama ifuatavyo.

7:Malengo na Mategemeo ya Warsha

- Malengo na mategemeo ya Warsha yatafafanuliwa kwa ufasaha zaidi na Mwezeshaji baada ya mimi kumaliza. Hata hivyo kwa kifupi malengo makubwa ya Warsha hii ni matatu:
  - Kuhakukusha kuwa wadau kateka warsha hii wanahusishwa kikamilifu kateka kuchangia mawazo na ushauri wao kuhusiana na mchakato mzima wa maendeleo wa Tanzania ili kujenga msimamo wa pamoja kuhusu Tanzania ya kesho
  - Kuanisha na kuchanganua mambo muhimu yanayohusu maendeleo ya nchi yetu baada ya mwaka 2015
  - Kutoa mapendekezo ya mambo muhimu na mikakati yenye tija kuliendeleza Taifa hili baada ya mwaka 2015

8:Mwongozo

- Maswali ya kutuongoza kwenye majadiliano yametayarishwa na wawezeshaji watakuwa karibu sana na wadau wakati wa majadiliano.
- Tunawaomba sana washiriki au wadau wetu kulisaidia hili kwa kuhakikisha kuwa mawazo na michango yenu mnaitoa yote, bila woga ili itusaidie kufikia matokeo ya warsha yetu.
- Tushiriki wote na tuwe wazi, na tuhakikishe tunayasoma kwa uangalifu sana na kuyaelewa maswali yanayoongoza majadilano. Wana-Warsha wawe huru kuuliza maswali kwa wawezeshaji muda wowote.

9:Hitimisho

- Kutokana na maelezo yaliyotolewa, utekelezaji wa majadiliano haya yanazingatia kanuni muhimu zilizopendekezwa na Kamati ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa. I) Kupanua wigo wa mashauriano ili kuhusisha wadau mbalimbali watakaoguswa na ajenda ya maendeleo baada ya 2015, na kusisitiza ushiriki wa watu ambao wamewekwa pembezoni katika michakato ya kutoa maamuzi. Lengo kubwa katika mchakato huu ni kusiakiliza sauti na mawazo ya vijana, watoto, waliowakilishwa kwa kiwango cha chini, maskini na wanyonge. ii) Kuhakikisha kuwa washiriki katika mashuriano wanapata taarifa muhimu zitakazoweza kutoa mrejesho wa kushangia taarifa ya kitaifa na kimataifa kuhusu 'hali ya maisha ya baadaye tunayoitaka'.

Mwisho

- Aksanteni Kwa Kunisikiliza